

MAKAO MAKUU

Ghorofa ya 4, Jengo la LAPF, Barabara ya Makole
S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania

Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005

Barua pepe: info@ewura.go.tz

Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

TANGAZO KWA UMMA

MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJI KUTOKA MAMLAKA YA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA SIKONGE (“SIKONGE WSSA”) KWA MWAKA 2018/19 – 2020/21

Maombi ya mabadiliko ya Bei Na. TR-W-18-003

Mnamo tarehe 13 Mei 2018 Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea maombi yaliyokamilika kutoka Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Sikonge (Sikonge WSSA) ya kutaka kuongeza bei ya huduma zake za majisafi kwa mwaka 2018/19 hadi 2020/21. Jedwali namba 1 hadi 6 hapa chini yanaonesha mchanganuo wa bei za sasa na zinazopendekezwa.

Jedwali Na 1: Bei za Sasa na Zinazopendekezwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi kwa Uniti moja ya ujazo)

Kundi la Wateja	Bei za Sasa	Bei Zinazopendekezwa					
	2017/18	Mabadiliko kwa asilimia	2018/19	Mabadiliko kwa asilimia	2019/20	Mabadiliko kwa asilimia	2020/21
Majumbani	800	75%	1,400	4%	1,450	3%	1,500
Biashara	935	64%	1,535	3%	1,585	3%	1,635
Taasisi	900	67%	1,500	3%	1,550	3%	1,600
Viwanda	-	-	-	-	-	-	-
Magati	1,000	400%	5,000	0%	5,000	0%	5,000

Jedwali Na.2: Tozo ya Huduma ya Sasa na Inayopendekezwa (Shilingi/Mwezi)

Kundi la Wateja	Tozo za sasa	Tozo Zinazopendekezwa					
	2017/18	Mabadiliko kwa asilimia	2018/19	Mabadiliko kwa asilimia	2019/20	Mabadiliko kwa asilimia	2020/21
Majumbani	0		1,000	0%	1,000	0%	1,000
Biashara	0		1,000	0%	1,000	0%	1,000
Taasisi	0		1,000	0%	1,000	0%	1,000
Viwanda	0		1,000	0%	1,000	0%	1,000
Kunyweshwa Mifugo	0		2,500	0%	2,500	0%	2,500

Jedwali Na.3: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshewa Huduma Baada ya Kukatiwa huduma (Shilingi/Kurejeshewa huduma)

Kundi la Wateja	Ada za Sasa	Ada zinazopendekezwa					
	2017/18	Mabadiliko kwa asilimia	2018/19	Mabadiliko kwa asilimia	2019/20	Mabadiliko kwa asilimia	2020/21
Majumbani	4,000	163%	10,500	0%	10,500	0%	10,500
Biashara	4,000	163%	10,500	0%	10,500	0%	10,500
Taasisi	4,000	163%	10,500	0%	10,500	0%	10,500
Viwanda	NA		25,000	0%	25,000	0%	25,000

Jedwali Na.4: Ada ya Maunganisho ya Huduma ya Maji ya Sasa na Inayopendekezwa (Shilingi kwa Maunganisho)

Kundi la Wateja	Ada za Sasa	Ada zinazopendekezwa					
	2017/18	Mabadiliko kwa asilimia	2018/19	Mabadiliko kwa asilimia	2019/20	Mabadiliko kwa asilimia	2020/21
Majumbani	15,000	33%	20,000	0%	20,000	0%	20,000
Biashara	15,000	67%	25,000	0%	25,000	0%	25,000
Taasisi	15,000	67%	25,000	0%	25,000	0%	25,000
Viwanda	15,000	67%	25,000	0%	25,000	0%	25,000
Kunywesha Mifugo	-		25,000	0%	25,000	0%	25,000

Jedwali Na.5: Kodi za Sasa na Zinazopendekezwa za Dira za Maji (Shilingi/Mwezi)

Kundi la Wateja	Kodi za Sasa	Ada zinazopendekezwa					
	2017/18	Mabadiliko kwa asilimia	2018/19	Mabadiliko kwa asilimia	2019/20	Mabadiliko kwa asilimia	2020/21
Majumbani	800	150%	2,000	0%	2,000	0%	2,000
Biashara	800	150%	2,000	0%	2,000	0%	2,000
Taasisi	800	150%	2,000	0%	2,000	0%	2,000
Viwanda	-		2,000	0%	2,000	0%	2,000

Jedwali Na.6: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Maombi ya Maunganisho Mapya ya Huduma ya Maji (Shilingi/Fomu)

Kundi la Wateja	Ada za Sasa	Ada zinazopendekezwa					
	2017/18	Mabadiliko kwa asilimia	2018/19	Mabadiliko kwa asilimia	2019/20	Mabadiliko kwa asilimia	2020/21
Majumbani	0		5,000	0%	5,000	0%	5,000
Biashara	0		5,000	0%	5,000	0%	5,000
Taasisi	0		5,000	0%	5,000	0%	5,000
Viwanda	0		5,000	0%	5,000	0%	5,000
Kunywesha Mifugo	0		2,500	0%	2,500	0%	2,500

Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Sikonge (Sikonge WSSA) imeeleza kuwa sababu za kuomba mapitio ya bei yanasababishwa na mapato madogo yanayotokana na bei za sasa ambazo hazikidhi gharama za utoaji wa huduma. Kwa mujibu wa Sikonge WSSA, ongezeko la bei linalopendekezwa litaiwezesha Mamlaka kumudu gharama za utoaji huduma na hivyo, pamoja na mambo mengine, kuongeza ubora wa maji, kuiwezesha Mamlaka kuwa endelevu na kuridhisha mahitaji ya wateja.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, kutakuwa na Mkutano wa Taftishi siku ya **Alhamisi, tarehe 14 Juni 2018 katika** Ukumbi wa **Chuo cha Maendeleo ya Jamii Sikonge** uliopo Sikonge mjini kuanzia saa **4:00 asubuhi** kwa ajili ya kupata maoni ya wadau ikiwa ni pamoja na Baraza la Ushauri la Serikali na Baraza la Ushauri la watumia Huduma zinazodhibitiwa na EWURA na wananchi wote kwa ujumla kuhusu uhalali wa bei zinazopendekezwa.

Wadau wanaopenda kutoa maoni kwa maandishi wanaombwa kufanya hivyo kwa kutuma maoni yao kwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa EWURA kwa anuani iliyoonesha hapo juu **ifikapo tarehe 20 Juni 2018**. Maelezo zaidi yanaweza kupatikana katika ofisi za **EWURA MAKAO MAKUU, GHOROFA YA NNE, JENGO LA LAPF; BARABARA YA MAKOLE, DODOMA** au **OFISI ZA MAMLAKA YA MAJI SIKONGE**.

Imetolewa na:
Kaimu Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)

25 Mei 2018